

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
27 Aprili, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AKUTANA NA RAIS MOHAMUD WA SOMALIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Viongozi wa Afrika hawana budi kudumisha umoja kama walivyodhamiria waasisi wa Umoja wa Afrika ili kuikaribia azma ya kujenga mtangamano.

Rais Samia amesema hayo leo wakati yeye na Mgeni wake Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia Mhe. Dkt. Hassan Sheikh Mohamud aliyepo nchini kwa ziara ya kiserikali ya siku mbili wakizungumza na vyombo vya habari katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, Ikulu.

Aidha, Rais Samia amesema licha ya Tanzania na Somalia kuwa na muingiliano kwa miaka mingi, ziara hiyo imetoa fursa ya kujadili na kuona umuhimu wa kuwa na mfumo rasmi wa kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Rais Samia pia amesema katika mazungumzo yao wamekubaliana kuimarisha mikutano ya mashauriano baina ya nchi hizo mbili kupitia mikutano ya wadau wa kisekta ili kuibua miradi ya ushirikiano yenye manufaa kwa wote.

Vile vile, Rais Samia amepongeza jitihada zinazofanywa na Rais Mohamud na Serikali yake katika kuendeleza vipaumbele vyake kitaifa na usimamizi wa ajenda ya ujenzi wa taifa la Somalia kupitia mashauriano ya kisiasa.

Rais Samia amemuhakikishia Rais huyo kuwa Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada za kurejesha amani nchini Somalia na iko tayari kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali.

Hii ni ziara ya kwanza kwa Rais Dkt. Hassan Sheikh Mohamud kufanya nchini Tanzania tangu nchi ya Somalia ijiunge na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

